

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA



Unapojibu tafadhali taja:
Kumb.Na.HMB/W:10/40/19

09 Juni 2023

Wananchi wote
Halmashauri ya Mji,
S.L.P. 219,
BUNDA.

**YAH: TANGAZO LA NAFASI 31 ZA KAZI YA MUDA YA KUKUSANYA
MAPATO KATIKA VYANZO MBALIMBALI VYA MAPATO
HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda anapenda kuwatangazia wananchi wote nafasi za Ajira ya muda ya kukusanya mapato katika vyanzo mbalimbali vya mapato katika Halmashauri ya Mji wa Bunda.

1.0. SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe Raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 45.
- Awe Mkazi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda.
- Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- Awe mwanifu katika kazi.
- Awe mwenye uwezo wa kufanya kazi eneo lolote ndani ya Halmashauri ya Mji wa Bunda.

2.0. MAJUKUMU

- Kukusanya na kupokea ada na ushuru katika eneo na chanzo alichopangiwa kwa viwango vilivyoainishwa na Sheria.
- Kuwasilisha makusanyo yote benki kwa wakati kulingana na Sheria ya fedha.
- Kutunza vitendea kazi na taarifa zinazohusu makusanyo.

3.0. MAOMBI YA AJIRA YAAMBATISHWE.

- Nakala ya cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha NIDA
- Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea.
- Picha mbili passport za sasa (moja ibandikwe kwenye barua ya maombi ya pili iambatishwe na na barua ya maombi).
- Barua ya Mdhamini pamoja passport mbili.

4.0 MALIPO

- Kiwango cha malipo kitaainishwa kwenye mkataba wako wa ajira.


5.0. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

- Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji wa Bunda,
288 Barabara ya Halmashauri,
S.L.P 219,
31582, BUNDA, MARA

**MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI HAYA NI TAREHE 23/06/2023 SAA 09:30
ALASIRI.**

Limetolewa na :


Emmanuel J. Mkongo
**MKURUGENZI,
HALMASHAURI Y MJI,
BUNDA.**

**TOWN DIRECTOR
BUNDA TOWN COUNCIL**

***NB: Tangazo hili linapatikana pia kwenye tovuti ya Halmashauri ya Mji wa Bunda
www.bundatc.go.tz, Instagram – bunda – town – Council na Twitter – bunda Town
Council.***